1.0 KITEGA UCHUMI CHA ROCK GARDEN MANISPAA YA MOROGORO

1.1 HISTORIA YA ENEO LA ROCK GARDEN

Bustani ya Rock Garden ilianzishwa kwa madhumuni ya kuwa ni sehemu ya mapumziko kwa Wananchi toka sehemu mbalimbali, iliitwa Rock Garden kutokana na uwepo wa mawe katika mto unaopita katika eneo hilo. Kitega uchumi hiki kipo katika makutano ya barabara ya Rwegasore na Boma pia ina eneo lenye ukubwa wa ekari nne (4) na kipo umbali wa kilometa tatu (3) toka katikati ya Mji.

Picha ya sehemu ya vivywaji katika eneo la Rock Garden

Madhari ya bustani hii ilitengenezwa na Mtaalam wa Kijapan anayeitwa Nauyuki Sawada mnamo mwaka 1984. Hata hivyo kazi ya kutengeneza eneo hili haikukamilika kwa asilimia mia moja kutokana na ufinyu wa fedha za kufanyia matengenezo hayo. Hivyo mtaalam huyu aliondoka baada ya muda wake kuisha na mradi ulisimama hadi mwaka 1987 ndipo Halmashauri iliamua kujenga jengo la muda kwa ajili ya kutolea huduma ya vinywaji kwa wageni waliokuwa wakifika katika eneo hilo.

Huduma hii ilikuwa ikisimamiwa na Halmashauri yenyewe hadi mwaka 1991 mradi huu ulikodishwa kwa muda kwa Morogoro Hotel Ltd. Baada ya mwaka 1993 Halmashauri ilikodisha mradi huu kwa Mtu mwingine na iliendelea kukodisha kila baada ya mkataba husika kwisha.

1.2 MAHALI ILIPO

Mradi wa bustani ya Rock Garden upo chini ya miteremko ya milima ya Uluguru na kando ya Mto Morogoro. Bustani hii iko ndani ya eneo la hifadhi ya mto Morogoro ni eneo zuri lenye kuvutia kwa shughuli za kitalii lenye bustani na mazingira ya uoto wa asili, pia ni sehemu zuri ya mapumziko katika siku za mwisho wa wiki na kwa shughuli mbalimbali za burudani.

Rock Garden imekuwa ni sehemu ya kivutio cha asili ndani ya Manispaa ya Morogoro ikiwa na mandhari nzuri ya kuvutia yenye asili ya milima ya Ulunguru, pia imekuwa ikitoa huduma ya uuzaji wa vinywaji vyenye kilevi na visivyo na kilevi, chakula, sehemu ya mapumziko na sherehe za wazi.

Picha ya madhari na uoto wa asili wa Rock Garden

1.3 HALI HALISI YA KIBIASHARA

Wateja wa kuu wa Rock Garden ni wakazi wa mji wa Morogoro na kutoka nje ya mkoa pamoja na watalii kutoka nchi mbalimbali wakiwa katika mapumziko yao mafupi.

1.4 HALI HALISI KWA SASA

Biashara inayofanyika kwenye bustani hii ni uuzaji wa vinywaji, burudani mbalimbali, ziara za kitalii, michezo ya watoto na chakula. Kwa sasa Rock Garden inaendeshwa na ndugu M/S Leornard. A. Mkonyi ambaye ameingia mkataba na Manispaa wa kuendesha kitega uchumi hiki kwa muda wa miaka mitatu. Mpangaji huyu atakuwa akiilipa Manispaa kiasi cha Tsh 750,000 .00 kila mwezi na mapitio ya kodi yatakuwa yakifanyika kila baada ya mwaka mmoja.

1.5 UTUNZAJI WA MAZINGIRA

Mazingira yaliyopo katika bustani hii yanatuzwa na kwa ushirikiano wa Halmashauri ya Manispaa na Mpangaji kama:

- Kufanya usafi eneo la bustani
- Kupanda miti ya asili
- Uimarishaji wa uzio katika eneo la bustani
- Ulinzi kuzunguka mipaka ya eneo la bustani

1.6 MPANGO WA UBORESHAJI WA ENEO HILI NI KAMA IFUATAVYO: -

1.6.1 Kujenga kituo cha habari kwa watalii (Tourist Information Centre)

Lengo kuu la kujenga kituo cha habari kwa watalii ni kuifanya Rock Garden kuwa ndio kituo kikuu cha kutoa taarifa na mwongozo wa safari za kitalii kwa watalii wa ndani na nje ya nchi ikiwa ni pamoja na kutangaza vivutio vilivyo ndani ya mkoa wa Morogoro katika kiwango cha kitaifa na kimataifa

Pia kituo hicho kitakuwa kikiratibu safari za kitalii katika mbuga mbalimbali za ndani ya mkoa na nje ya mkoa kwa wageni watakao hitaji uratibu wa safari zao

1.6.2 Kujenga mgahawa wa kisasa (Restaurant)

Mgahawa utahudumia wateja wa kila siku pamoja na wale wasemina mbalimbali zitakazofanyika katika eneo la Rock Garden, pia kuhudumia wageni wa kitalii wa ndani na nje ya nchi ambao watapenda kufanya mapumziko mafupi katika eneo la Rock Garden

1.6.3 Kujenga banda kubwa la makuti

Kulingana na mazingira ya eneo la Rock Garden upo umuhimu wa kujenga Banda kubwa la Makuti lenye uwezo wa kuhudumia watu 100 watakaohitaji kufanya semina, mikutano na sherehe katika sehemu ya wazi bila kupata usumbufu wa mvua au jua.

1.6.4 Kuweka uzio imara kuzunguka lote la Mradi

Uzio wa kuzunguka eneo ni muhimu ili kuimarisha ulinzi na kuweka mazingira bora ya usalama wa mali za wateja na Rock Garden kwa ujumla.

Pia uzio wa kuzunguka eneo utaimarisha udhibiti wa mapato wa mapato ya mlango wakati wa matanasha yatakayohusisha kiingilio cha mlangoni

1.6.5 Ukarabati wa eneo la Bar

Eneo la bar limekuwepo kwa muda mrefu bila kufanyiwa ukarabati mkubwa ili kuliweka katika ubora na mazingira ya kuvutia kibiashara hivyo malengo ni kulikarabati eneo lote la bar ili kulirudisha katika ubora na hali nzuri ya kuvutia kibiashara inayoendana na mazingira halisi ya soko la biashara ya bar. Ukarabati utahusisha vyoo, paa la kwenye bar na upakaji wa rangi katika eneo la bar

1.6.6 Bwawa la kuogelea (Swimming Pool)

Ili kulinda ubora wa mazingira ya mto morogoro na kuepusha uchafuzi wa maji yanayo tiririka katika mto huo ambao unapita katika eneo la Rock Garden, ipo haja ya kujenga bwawa la saizi ya kati (10M*7M) kwa ajili ya kuongelaea. Hivyo wateja wote ambao watapendelea kuogelea watalitumia bwawa hilo na kuufanya mto morogoro kubaki katika hali ya usafi

1.6.7 Nyumba ya kupumzikia wageni (Rest House)

Lengo ni kujenga nyumba ndogo ya vyumba vitatu vinavyojitosheleza (self-contained) kwa ajili ya mapumziko kwa wageni watakao penda kufanya mapumziko mafupi ndani ya eneo la rock garden kabla ya kuendelea na safari zao za kitalii. Hii itawarahisishia wageni ambao watakuwa wakiratibiwa safari zao za kitalii na kituo cha habari za kitalii cha Rock Garden kwa kupata sehemu ya mapumziko wakiwa wanasubiri mpangilio wa ratiba za safari

1.6.8 Sehemu ya kuchezea watoto (Kids Corner)

Lengo ni kuhakikisha watoto pia wanapata sehemu iliyo bora na salama kwa kuchezea, hii itahusisha kuweka vifaa mbalimbali vya kisasa kwa ajili ya michezo ya watoto

1.6.9 Ukumbi wa mkutano (Conference Hall)

Malengo ni kuweka ukumbi wa kisasa wa mikutano wenye uwezo wa kuhudumia watu hamsini (50) kwa wakati mmoja, hili linatokana na hali halisi kuwa mkoa wa Morogoro umekuwa sehemu ya katikati ya nchi inayoweza kufanya watu wengi kuweza kukutana kwa urahisi katika mikutano ya kikazi, kibiashara.

1.6.10 Ujengaji wa vyoo vya kisasa vinne, kati ya hivi viwili vitakuwa VIP na viwili vitakuwa vya kawaida.

1.6.11 Kuboresha maegesho ya magari ili tuweze kupaki magari mengi kwa wakati mmoja.

John K. Mgalula
MKURUGENZI WA MANISPAA
MOROGORO